

TANGAZO LA SERIKALI NA. 66 la tarehe 24/02/2012

SHERIA YA MABADILIKO YA KATIBA YA MWAKA
(NA. 8 YA MWAKA 2011)

TANGAZO

(Limetolewa chini ya kifungu cha 6)

KWA KUWA, kifungu kidogo cha (1) na (2) cha kifungu cha 6 cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka, 2011 kinampatia mamlaka Rais, baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar na kwa kuzingatia msingi wa usawa wa wajumbe kutoka kila upande wa Jamhuri ya Muungano kuteua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, na wajumbe wengine wa Tume wasiopungua ishirini na wasiozidi thelathini kama inavyoelekezwa na kifungu cha 7(1);

NA KWA KUWA, katika kufanya uteuzi wa wajumbe wa Tume atalazimika kutilia maanani:

- (a) uzoefu katika kufanya mapitio ya katiba na sifa za kitaaluma za wajumbe kwenye mambo ya katiba, sheria, utawala, uchumi, fedha na sayansi ya jamii;
- (b) jiografia na mtawanyiko wa watu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na
- (c) umri, jinsia na uwakilishi wa makundi mbalimbali ya kijamii;

NA KWA KUWA, vifungu vidogo vya (4) na (5) vya kifungu cha 6 vinaeleza kwamba mtu hatakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa mjumbe wa Tume isipokuwa kama ni mwaminifu wa hali ya juu na ana tabia isiyotiliwa mashaka na jamii na mtu huyo si mtumishi katika vyombo vya usalama au si raia wa Tanzania;

NA KWA KUWA, kifungu kidogo cha (6) cha kifungu cha 6 kinamtaka Rais kualika vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu, jumuiya za dini, asasi za kiraia, jumuiya, taasisi na makundi mengine ya watu yenye malengo yanayofanana kuwasilisha kwa Rais orodha ya majina ya watu kwa ajili ya kuteuliwa kuwa wajumbe na ambayo itaonyesha umri, jinsia, uzoefu, sifa na mahali mtu huyo anapoishi;

NA KWA KUWA, Rais ana nia ya kuwateua wajumbe wa Tume kwa kuzingatia masharti ya sheria;

HIVYO BASI, MIMI, JAKAYA MRISHO KIKWETE, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa masharti ya kifungu cha 6(6) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, 2011, NATOA tangazo lifuatalo:

Jina 1. Tangazo hili litaitwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (Mwaliko wa Orodha ya Majina)(Wajumbe wa Tume) la mwaka, 2012.

Mwaliko wa orodha ya majina 2.-(1) Tangazo la Mwaliko unatolewa kwa vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu, jumuiya za dini, asasi za kiraia, jumuiya, taasisi na makundi mengine ya watu yenye malengo yanayofanana kuwasilisha kwa Rais orodha ya majina ya watu watakaoteuliwa kuwa wajumbe wa Tume.

(2) Orodha ya majina itakayowasilishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), itapaswa kuwa na majina yasiyozidi matatu na itaonyesha umri, jinsia, uzoefu, sifa na mahali anapoishi kila mtu aliyemo katika orodha.

Muda wa kuwasilisha orodha 3. Kipindi ambacho orodha ya majina itawasilishwa kwa Rais kwa mujibu wa aya ya 2, kitakuwa ni siku ishirini na moja zitakazohesabika kuanzia tarehe 25 Februari, 2012 na kitakoma tarehe 16 Machi, 2012.

Kuwasilisha orodha 4.-(1) Orodha ya majina itawasilishwa kwa Rais kwa maandishi ama moja kwa moja kwa mkono au kwa rejista ya posta kupitia anuani kama ifuatavyo:

Ama: Katibu Mkuu Kiongozi,
Ikulu,
S.L.P. 9120,
DAR ES SALAAM.

Au: Katibu wa Baraza la Mapinduzi na
Katibu Mkuu Kiongozi;
Ofisi ya Rais,
S.L.P. 4224,
ZANZIBAR.

(2) Tangazo hili litakoma tarehe 16 Machi, 2012.

KWA AMRI YA RAIS

Dar es Salaam,
24 Februari, 2012

PENIEL M. LYIMO,
Kaimu Katibu Mkuu Kiongozi